

WeProsper: Muungano wa Kimataifa wa Uwezeshaji wa Wanawake Kiuchumu

WeProsper ni muungano wa kimataifa unaoendeleza uwezeshaji wa wanawake kiuchumi (WEE) kwa kujihusisha na utetezi wa kimkakati ili kuendeleza usawa wa kijinsia, kushughulikia vikwazo vyta kimuundo, na kukuza sauti na nguvu za wanawake na wasichana kama washirika muhimu katika uchumi. Tunashirkiana, ili kujenga na kutumia msingi wa ushahidi wa kimataifa kuhusu uwezeshaji wa wanawake kiuchumi kwa kutumia mbinu ya utetezi wa haki za wanawake na mwiningiliano wa utambulisho ili kubuni sera ya kimataifa, kuongeza ufadili kwa WEE, na kuunga mkono ustawi wa wanawake na wasichana katika utofauti wao wote.



Wakati Muhimu kwa Uwezeshaji wa Wanawake Kiuchumi

Uwezeshaji wa Wanawake kiuchumi (WEE) ni muhimu kwa haki za wanawake, kwa ustawi, ushawishi, mamlaka, na usawa wao, na pia kwa mafanikio ya biashara na uchumi. Hata hivyo, ikilinganishwa na ukosefu wa usawa wa kijinsia katika elimu na afya ambaa umepungua, ukosefu wa usawa wa kijinsia katika ushiriki wa kiuchumi na fursa za kiuchumi umesalia kuwa kubwa na uliochukua muda mrefu, hata kabla ya COVID-19. Baraza la Uchumi Duniani linakadiria kuwa kwa kutumia kiwango cha sasa, itachukua miaka 276.6 ili kuziba pengo hili la ukosefu wa usawa wa kijinsia. Zaidi ya hayo, COVID imerudisha nyuma mafanikio ambayo yalikuwa yamefikiwa baada ya juhudini kubwa duniani kote katika uwezeshaji wa wanawake kiuchumi, ukiathiri kazi za wanawake, biashara, kazi za utunzaji zisizo na malipo, upatikanaji wa fedha na rasilimali muhimu, na viwango vya umaskini. Ni wakati muhimu wa kuunga mkono WEE – ili wanawake na familia zao wapate riziki, kuhakikisha ufuufuaji wa uchumi ulio shirikishi na endelevu, na kuhakikisha kuwa hatua zinapigwa katika kufikia usawa wa kijinsia.

WeProsper ilibuniwa ili kuchochea hatua za kimataifa katika uwezeshaji wa wanawake kiuchumi katika wakati huu muhimu wa kukabiliana na COVID na katika mwongo wa utendakazi mwingi ili kufikia Malengo ya Maendeleo Endelevu na ajenda ya 2030 ya Umoja wa Mataifa.. Tunaamini kwamba lazima sera na ufadhili uimarishwe zaidi kuliko hapo awali ili kuzuia vikwazo, na vilevile ili kuanza kuona maendeleo makubwa katika mbinu za kujipatia riziki, fursa, na haki ya kiuchumi na haki za wanawake na wasichana duniani kote. Uanachama wetu wa kimataifa unajumuisha kundi lenye uanuwai wa zaidi ya mashirika 30 ya uraia ya ndani, ya kikanda, na ya kimataifa, taasisi za kitaaluma, mashirika ya kutetea haki za binadamu, makundi yanayoongozwa na wanawake na yanayotetea haki za wanawake, na mashirika ya sekta ya kibinafsi ambayo yanazingatia masuala katika wigo wa WEE. WeProsper umeungana na sekta zote na ulimwengu wote ili kutumia kina na upana wa maarifa na uzoefu wetu ili kuleta utetezi wa kimkakati wa WEE kuitia mapendekezo ya sera yenye msingi wa ushahidi uliotokana na uchunguzi na ufadhili.



Picha: Paula Bronstein/Getty Images//Picha za Uwezeshaji, India

WeProsper inaongozwa na kanuni zifuatazo:

	<p>1</p> <p>Kutumia mbinu ya utetezi wa haki za wanawake, na mwingiliano wa utambulisho</p>		<p>2</p> <p>Kuunganisha na kuinua ukuaji wa kijumla wa WEE</p>
<p>3</p> <p>Kukabili vikwazo vya kimundo na vya kimfumo kwa WEE</p>		<p>4</p> <p>Kujenga uwezo na kuimarisha sauti za wanawake katika Nchi zenyenye Mapato Duni na Kati</p>	
	<p>5</p> <p>Kujenga na kutumia msingi wa ushahidi wa kimataifa kuhusu WEE</p>		<p>6</p> <p>Kushiriki katika utetezi wa kimkakati, unaotegemea ushahidi</p>
<p>7</p> <p>Kuwezesha michakato ya kiuchumi na maendeleo iliyo shirikishi na endelevu</p>		<p>8</p> <p>Kukuza uwajibikaji</p>	

Uzinduzi wa Muungano wa Kimataifa wa Uwezeshaji wa Wanawake Kiuchumi

Mbinu ya Ujumla ya WeProsper kwa WEE

WeProsper inatambua kuwa uwezeshaji wa wanawake kiuchumi unafafanuliwa kwa njia nyingi tofauti, lakini mara nyingi, fasili hizi ni finyu sana na husababisha mbinu za vitengo vidogo vidogo kwa WEE ambazo hazishughulikii masuala ya kimuundo na masuala yanayohusiana na haki. Ushahidi uko wazi: bila kushughulikia masuala ya kimuundo na kuunga mkono haki zao, maendeleo kwenye WEE yatakwama. WeProsper unachukua mtazamo kamili kwa WEE, ambao haulengu tu kuwaingiza wanawake kwenye nafasi za ajira au kuwaunga mkono kama wajasiriamali (ingawa hizi ni sehemu muhimu za WEE), bali kushughulikia masuala ya kimuundo na ya kimfumo ambayo hubaini matokeo ya uchumi. Haya ni pamoja na:

Miundo ya kijamii:

Kanuni za jinsia: Kanuni kuhusu ugavi wa kazi kwa misingi ya kijinsia, kazi "zinazowafaa" wanawake, na hali ya chini ya wanawake inazuia uwezo wao wa kupata kazi zenye staha na kuendeleza unyanyasaji wa kijinsia, pamoja na athari za kiuchumi na athari kwa ustawi wao katika maisha yao yote.

Kazi ya utunzaji isiyo na malipo: Ulimwenguni, majukumu ya kazi ya utunzaji isiyo na malipo huwazuia asilimia 42 ya wanawake, na asilimia sita pekee ya wanaume, kufanya kazi yenye malipo na huchangia siku ndefu za kazi na ukosefu wa wakati wa kupumzika na kujipurudisha kwa wanawake.

Nafasi za ajira:

Ukosefu wa usawa wa kijinsia katika maeneo ya kazi: Ubaguzi, vikwazovya kisheria, na majukumu mengi ya utunzaji na kazi za nyumbani zisizo na malipo huwafanya wanawake wengi kung'ania nafasi chace za kazi, mara nyingi katika ajira hatarishi, na yenye athari mbaya kwa malipo, marupurupu, na mazingira ya kazi.

Kazi nzuri: Wengi wa wafanyakazi wanawake wako katika sekta ya juu kali, wanakosa kulindwa na sheria zinazowalinda wafanyakazi na kupata faida kama vile pensheni, bima ya afya, au likizo ya ugonjwa. Ukosefu wa usawa wa kijinsia katika mishahara umeendelea kuwa donda sugu, hali kadhalika ubaguzi na unyanyasaji, ambao unawanyima kazi zenye staha. Asilimia 50 ya wanawake wanakabiliwa na ubaguzi, dhuluma, na unyanyasaji kazini katika maisha yao.

Haki za kisheria:

Haki za ardhi: Ukosefu wa usawa katika haki za ardhi, ikiwa ni pamoja na sheria kuhusu urithi, huchangia ukosefu wa usawa wa kijinsia katika umiliki wa ardhi, ambao mara nyingi ndio tegemeo kuu la kupata riziki. Wanawake wanamiliki katika 5-20% ya ardhi ya kilimo katika nchi zinazoendelea.

Haki za kiuchumi: Wanawake wana robo tatu pekee ya haki za kisheria ikilinganishwa na wanaume zilizo muhimu kwa kujumuishwa kiuchumi, kama vile malipo sawa kwa kazi sawa na wanakabiliwa na sheria zinazowazuia kuajiriwa katika taaluma fulani.

Sera za uchumi wa kiwango cha juu:

Uwezo wa kifedha: Kuendeleza WEE kunahitaji ufadhili mkubwa kutoka kwa serikali, na vipengele vingi vya sera ya uchumi wa kiwango cha juu ni muhimu ili kuhakikisha kuwa kuna uwezo wa kifedha kwa uwekezaji huu, ikiwa ni pamoja na sera za kodi, fedha, bajeti na udhibiti wa deni.

Mpango wa kuruzuku jamii: Muundo wa mifumo ya kuruzuku jamii ni muhimu katika kubainisha iwapo wanawake wana ufikiaji sawa na rasilimali za kuwasaidia kupata riziki yao, hasa ikizingatiwa kuwa katika nchi nyingi, wanawake wengi wako katika sekta ya uchumi isiyo rasmi.

Kujenga na Kutumia Msingi wa Ushahidi wa Kimataifa kwenye WEE

Uanachama wa WeProsper unaotoka kwenye sekta mbalimbali unatupa ushahidi mwingu, na tunafanya kazi kwa pamoja ili kuunganisha aina mbalimbali za utafiti na ushahidi kutoka kwa uzoefu wa wanawake, wasichana, na makundi yaliyotengwa kihistoria kutoka duniani kote. Uwezeshaji wa wanawake kiuchumi ni mada changamano yenye vipengele vingi inapotazamwa kwa ujumla, unaohitaji viashirio thabiti na data ya jinsia tofauti ili kupima vipengele hivi na kutathmini mabadiliko ambayo yametokea kwa wakati fulani. Wanachama wetu wamejitolea katika utetezi wa data bora zaidi ya jinsia, na tunashiriki katika mijadala nzuri kuhusu kipimo cha WEE, kama vile Ushirikiano wa Mafunzo ya Umuhimu wa Zana na Viashirio vya Kipimo cha WEE. Juhudi hizi hujenga maarifa mengi na ya kina, ambayo kutoptokana nayo tunafanya kazi kama daraja muhimu kutoka kwa utafiti hadi kubuniwa kwa sera, kubuni mapendekezo yanayotokana na utafiti ambayo huwawezesha watungaji sera kuharakisha maendeleo ya WEE ipasavyo.

Kushirikiana Ulimwenguni ili Kuharakisha Maendeleo katika WEE

Kwa mtazamo wetu wa kijumla, unaotegemea ushahidi na uanachama anuwai, WeProsper uko tayari kupanua mtazamo wake na kuboresha mazungumzo kuhusu WEE katika ngazi ya kimataifa, ikiangazia kwa kina vipengele mahususi vya muktadha na ukosefu wa usawa unaowakumba makundi mengi ya wanawake na wasichana. Ni muhimu kuangazia njia ambazo rangi, kabilia, tabaka, uraia, ulemavu, dini, mwelekeo wa kijinsia, utambulisho wa kijinsia na umri, mionganoni mwa mambo mengine, huingiliana ili kubainisha matokeo ya kiuchumi kwa wanawake na wasichana. Muungano wetu wa kimataifa hufanya kazi kwa karibu na miungano ya nchi na ya kikanda na mashirika ya mashinani ili kuhakikisha kwamba vipimo hivi vya WEE, pamoja na vipengele vya mazingira wezeshi vya eneo fulani na nchi mahususi, vinatumika kubuni mapendekezo yetu yanayotegemea ushahidi na utetezi wa kimkakati.

WeProsper inajihuisha na utetezi wa kimkakati kwa:

- Mifumo endelevu na shirikishi ya kiuchumi, ambayo inaunga mkono kazi na mbinu za kujipatia riziki zenye staha na umiliki sawa wa mali;
- Kazi ya utunzaji kutambuliwa, kutuzwa, kuwakilishwa, na kugawanywa kwa usawa katika wanafamilia na katika familia na serikali;
- Wanawake na wasichana katika uanuwai wao wote wawe na uwezo na usemi sawa katika kufanya maamuzi, ikiwa ni pamoja na uhuru kutoka kwa unyanyasaji na dhuluma, kuhusika katika maamuzi ya kuchagua shughuli za kiuchumi wanazoshiriki, fidia ya haki, na ufikiaji sawa wa kile ambacho wanahitaji ili kuishi, na kustawi; na
- Watunga sera na taasisi za kimataifa kuangazia kwa kina mahitaji ya wanawake na wasichana na kubuni, kutekeleza, na kufadhilli masuluhisho shirikishi, yenye msingi wa ushahidi, ya utetezi wa haki za wanawake, ya mwingiliano na ya mageuzi ya kijinsia kwa changamoto zinazowakabili.



Picha: Jonathan Torgovnik/Getty Images, Ghana

Jiunge Nasi ili Tupige Hatua Kubwa

Sauti na uzoefu zaidi huimarisha utetezi wetu zaidi katika wakati huu muhimu. WeProsper unaalika mashirika ya kiraia ya ndani, kikanda na kimataifa, taasisi za kitaaluma, mashirika ya utetezi, makundi yanayoongozwa na wanawake na yanayotetea haki za wanawake, na mashirika ya sekta ya kibinafsi ambayo yanependa kuchangia katika lengo na maono ya pamoja ya muungano kuijunga nasi! Wanachama wa Muungano

hushiriki maarifa mara kwa mara kuitia barua pepe na hukutana kila baada ya miezi mitatu; vikundi vyetu vya kazi vinapanga mikakati ya utetezi na ya kuitisha ujumbe, kushiriki maarifa na utafiti, na kuongeza maarifa na uwezo wao kuhusu WEE.

**Kwa maelezo zaidi na kujinga,
wasiliana na Kelsey Harris (kharris@icrw.org)**

Maelezo ya mwisho

1. International Labour Organization (2017). [Economic Impacts of Closing the Gender Gap](#).
2. World Economic Forum (2021). [Global Gender Gap Report 2021](#).
3. O'Donnell, Megan, Mayra Buvinic, Charles Kenny, Shelby Bourgault, and George Yang (2021). [Promoting Women's Economic Empowerment in the COVID Context](#). Center for Global Development, Working Paper 575.
4. Buschmann, Mareen and Sarah Fuhrman (2020). [COVID-19 Could Expose Women to Decades of Poverty: Implications of the COVID-19 Pandemic on Women's and Girls' Economic Justice and Rights](#). Care International.
5. Simon Fraser University Gender and COVID-19 Research Project. [Gender Analysis and COVID-19 Matrix](#).
6. United Nations Sustainable Development Group. [Decade of Action](#).
7. Noble, Rachel, Rachel Walker, Lila Caballero, and Asha Herton (2020). [Another World is Possible: Advancing feminist economic alternatives to secure rights, justice and autonomy for women and a fair, green, gender equal world, Volume 1](#). ActionAid.
8. Grantham, Kate, Dana Stefov, and Rebecca Tiessen (2019). [A Feminist Approach to Women's Economic Empowerment: How Canada Can Lead on Addressing the Neglected Areas of WEE](#). Oxfam Canada.
9. Kidder, Thalia, Sophie Romano, Claudia Canepa, John Chettleborough, and Celeste Molina (2017). [Oxfam's Conceptual Framework on Women's Economic Empowerment](#). Oxfam International.
10. Marcus, Rachel (2018). [The norms factor: Recent research on gender, social norms, and women's economic empowerment](#). International Development Research Center.
11. Wamue-Ngare, Grace, Pacificah Okemwa, Simon Miruka, Lucy Maina, Pauline Kamau, Grace Okong'o, Jane Njuguna, Isaac Kimunio, Lillian Kiruja, and Simon Peter Okoth (2021). [Impact of programmes and Initiatives addressing Sexual and Gender-Based Violence as a constraint to Women Economic Empowerment](#). Kenyatta University Women's Economic Empowerment Hub.
12. Lawson, Max, Anam Parvez Butt, Rowan Harvey, Diana Sarosi, Clare Coffey, Kim Piaget and Julie Thekkudan (2020). [Time to Care: Unpaid and underpaid care and the global inequality crisis](#). Oxfam International.
13. Addati, Laura, Umberto Cattaneo, Valeria Esquivel, and Isabel Valarino (2018). [Care Work and Care Jobs for the Future of Decent Work](#). International Labour Organization.
14. Better Work (2022). [Gender Equality in the Global Garment Industry: Highlights of the Better Work Strategy 2018–2022](#). International Labour Organization and International Finance Corporation.
15. Bonnet, Florence, Vicky Leung, and Juan Chacaltana (2018). [Women and Men in the Informal Economy: A Statistical Picture](#). International Labour Organization.
16. Nayak, Nilini (2021). [Domestic Workers Organize for their Recognition and Rights: The SEWA Process](#). Self-Employed Women's Association.
17. Khokhar, Tanya (2021). [Ending Gender-Based Violence and Harassment in the World of Work: The Critical Importance of Implementing ILO Convention 190](#). International Center for Research on Women.
18. Landesa (2012). [Women's Secure Rights to Land: Benefits, Barriers, and Best Practices](#).
19. World Bank Group (2021). [Women, Business, and the Law 2021](#).
20. Woodroffe, Jessica and Chiara Capraro (2016). [Breaking down the barriers: Macroeconomic policies that promote women's economic equality](#). Gender and Development Network.
21. UN Women (2017). [Macroeconomic Policy and Women's Economic Empowerment](#).
22. International Labour Organization (2019). [Universal social protection for human dignity, social justice and sustainable development](#). International Labour Conference, 108th Session.
23. Cookson, Tara, Rita Sandoval, Silke Staab, and Constanza Tabbush (2021). [Putting gender equality at the centre of social protection strategies in sub-Saharan Africa: How far have we come?](#) UN Women.
24. Buvinic, Mayra, Megan O'Donnell, James C. Knowles, and Shelby Bourgault (2020). [Measuring Women's Economic Empowerment: A Compendium of Selected Tools](#). Center for Global Development and Data2X.
25. Data2X (2021). [It's Time to Make Bold Commitments to Gender Data](#).
26. [The Women's Economic Empowerment \(WEE\) Measurement Learning Collaborative](#). Center For Global Development.
27. de Hoop, Thomas, Amber Peterman, and Leigh Anderson (2020). [Guide for Measuring Women's Economic Empowerment and Economic Outcomes in Impact Evaluations of Women's Groups](#). Evidence Consortium of Women's Groups.

Wanachama wa Muungano



actionaid



APCO
worldwide®

BFA
GLOBAL



data2x



IDinsight



Landesa

S H E
STYLE HER EMPOWERED



MARKETSHARE
ASSOCIATES

OXFAM
Canada

The Asia Foundation

Serve Tanzania
Foundation

SEWA BHARAT



URGENT
ACTION
FUND +
AFRICA
FOR WOMEN'S HUMAN RIGHTS

WORLD Policy
Analysis Center



WOMEN'S
REFUGEE
COMMISSION
Women. Refugees. Resilience.



Machi 2022